JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Simu Nambari: 2150043 – 6/2150360

11102 ILALA

Fax No: (022) 2150047

E-mail:dgeneral@pccb.go.tz

ILALA – JANUARI 15, 2021

TAARIFA KWA UMMA

UTENDAJI WA TAKUKURU MKOA WA ILALA KWA KIPINDI CHA OKTOBA HADI DESEMBA, 2020

NDUGU WANAHABARI.

Ninapenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana kwa kuitikia wito wetu na kuja kushiriki kwenye mkutano huu. Karibuni sana ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Ilala.

NDUGU WANAHABARI.

Ni utaratibu wetu TAKUKURU kutoa taarifa ya utendaji kazi kwa umma katika kipindi cha kila robo mwaka kupitia kwenu wanahabari. Leo TAKUKURU Mkoa wa Ilala tunatoa taarifa ya utendaji kazi kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2020. Kama inavyofafanuliwa hapa: -

1.0. MAHAKAMA

Katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2020 Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Ilala inaendelea na mashauri 22 Mahakamani ikiwa ni pamoja na mashauri mapya mawili yaliyofunguliwa kipindi hiki kama ifuatavyo:

Mamlaka ya Mapato (TRA) Mashauri 4, Idara ya Afya mashauri 4, Serikali za Mitaa mashauri 2, Wanasiasa mashauri 2, Idara ya Ardhi shauri 1, DAWASA shauri 1, aliyekuwa mtumishi wa TAKUKURU shauri 1, wafanyabiashara mashauri 4, Ujenzi (TANROARDS) Shauri 1 na Elimu ya Juu Mashauri 2.

2.0. UCHUNGUZI

Katika kipindi hicho pia TAKUKURU Mkoa wa Ilala tumepokea taarifa 247 katika taarifa hizo malalamiko yaliyohusu rushwa ni 68, ambapo idara zililizolalamikiwa zaidi ni Serikali za Mitaa taarifa 16, Mahakama ni 12, Polisi 07, Elimu 06, Ardhi 07 na Afya 03, uchunguzi wa taarifa hizi unaendelea katika hatua mbalimbali.

- Pia katika kipindi hiki uchunguzi umeweza kuokoa nyumba ya mwananchi aitwaye CHARLES RWEYEMAMU ambaye nyumba yake yenye thamani ya Tsh. 140,000,000/= iliyokuwa katika kiwanja namba 733 Block A YOMBO VITUKA ilitumika kama dhamana ya ndugu PETER NGOSI MASIGAZWA aliyekopa Tsh 60,000,000/= katika benki ya NMB Tegeta mwezi Agosti 2016. Baada ya kupata mkopo huo alifanya marejesho mara moja tu, hivyo kupeleka nyumba hiyo kuuuzwa kwa mnada na benki ya NMB kwa lengo la kufidia fedha zake. Uchunguzi ulifanikiwa kuona dosari zilizojitokeza na kupelekea ndugu Peter kumkabidhi ndugu Rweyemamu nyumba yake iliyopo GOBA KULANGWA karibu na kanisa la EAGT kama fidia ya kupoteza nyumba yake. .

- Uchunguzi umefanikiwa kuokoa bajaji tano kutoka kwa mfanyabiashara mwenye kampuni iitwayo ELGON TRADERS yenye ofisi zake BUZA, Temeke. Kikundi kiitwacho KIKUNDI CHA WALEMAVU NA MAENDELEO (KWAMI) walitoa fedha kiasi cha Tsh. 36,000,000/= tarehe 28/05/2020 lakini hawakupatiwa bajaji hizo na mfanyabiashara huyo hadi

Ofisi ya TAKUKURU (M) Ilalailipoingilia kati suala hili, na mnano tarehe 27/11/2020 mfanyabiashara alikabidhi bajaji mbili aina ya TVS ofisi za TAKUKURU Ilala na bajaji tatu zilizobaki atazileta siku chache zijazo ili nasi tuweze kuwakabidhi walemavu hao wa kikundi cha KWAMI.

- TAKUKURU Mkoa wa Ilala imekuwa ikipokea taarifa na kufanya chunguzi mbalimbali kuhusu baadhi ya waajiri wa sekta binafsi kutokulipa pesa za mafao ya watumishi wao katika mfuko wa jamiii wa NSSF kwa wakati hivyo kupelekea waajiriwa kukosa stahiki zao na kupata usumbufu kipindi wanapostaafu au kuvunja mikataba na waajiri wao.

  Napenda kutoa wito kwa waajiri wote kupeleka fedha za mafao ya watumishi kwa wakati kwani kuacha kufanya hivyo ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria za nchi.

Aidha TAKUKURU Mkoa wa Ilala imeweza kudhibiti upotevu wa fedha kiasi cha Tsh. 543,305,567 /= kutoka kwa wadaiwa sugu wa Vikoba,Saccos na fedha husika kupatiwa Saccos na vikoba husika.

Katika kipindi cha robo mwaka kijacho (Oktoba hadi Desemba 2020) Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Ilala inategemea kukamilisha chunguzi mbalimbali zinazohusu wananchi kudhulumiwa mashamba yao, ukwepaji wa kodi wa zaidi ya shilingi Bilioni 7, rushwa kwenye zoezi la kupangiwa vituo vya kazi, ubadhirifu wa fedha za serikali kupitia manunuzi ya Umma zaidi ya shilingi Bilioni 11 nk.

3.0. UELIMISHAJI UMMA

TAKUKURU pia tunalo jukumu la Uelimishaji Umma. Katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2020 Dawati la Elimu kwa umma Mkoa wa Ilala tumeweza kuelimisha makundi mbalimbali kwa njia ya vipindi vya redio na

TV, semina,mikutano ya hadhara, mikutano na waandishi wa habari. Kwa kushirikiana na baadhi ya wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), ambao wanafanya mafunzo kwa vitendo TAKUKURU, tumefanikiwa kufungua na kuimarisha klabu za wapinga rushwa katika shule za msingi na sekondari.

4.0. UZUIAJI RUSHWA

Katika kuhakikisha kuwa kero mbalimbali zinapatiwa ufumbuzi, na wakati mwingine kubaini mianya ya rushwa na hatimaye kupata njia sahihi ya kuishauri serikali kuhusiana na masuala ya rushwa katika mkoa wetu tumefanikiwa kufanya yafuatayo:

i. Warsha ya kujadili matokeo ya uchambuzi wa mfumo wa usimamizi wa kodi za huduma (service levy) Manispaa ya Ilala.

ii. Kuandaa taarifa ya uchambuzi ya uendeshaji wa uchaguzi Mkuu wa Rais,Wabunge na Madiwani kwa mwaka 2020.

iii. Ufuatiliaji wa mitihani ya kidato cha pili iliyoanza tarehe 09/11/2020 hadi tarehe 20/11/2020 na kidato cha nne iliyoanza tarehe 23/11/2020 kwa kukusanya taarifa mbalimbali kuhusu ufanyikaji wa mitihani hiyo.

iv. Kuandaa taarifa ya uendeshaji wa mitihani ya kidato cha pili na kidato cha nne mwaka 2020 katika halmashauri ya Manispaa ya Ilala.

MWISHO

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa kukubali kuja kunisikiliza na hasa tukizingatia umuhimu wa shughuli yenu ya habari, napenda kutoa wito kwenu kuendelea kutoa elimu juu ya adui rushwa kwa jamii. TAKUKURU inawaomba mkaendelee kuwa mabalozi madhubuti wa mapambano dhidi ya rushwa.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA

IMETOLEWA NA

Christopher Myava

KAMANDA WA TAKUKURU (M) ILALA